

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA**

**MJKOA WA MARA:**

Simu Na.028 2621055

Nukushi .Na.0282621264

Barua pepe: [ded@bundadc.go.tz](mailto:ded@bundadc.go.tz).

Tovuti [www.bundadc.go.tz](http://www.bundadc.go.tz)

**Unapojojibu tafadhalil taja:**

Kumb. Na. HB/JB/W : 20/63



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P 126,  
**BUNDA.**

23 Novemba, 2020.

**TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA KWA NAFASI MLINZI DARAJA LA II**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kujaza nafasi tatu (03) za ajira ya mkataba kwa nafasi ya ulinzi. Yeyote mwenye sifa anaruhusiwa kutuma maombi.

**SIFA ZA MUOMBAJI.**

- Awe mhitimu wa kidato cha nne na kufuzu mafunzo ya mgambo, Polisi, JKT, Jeshi la Wananchi au mafunzo ya zimamoto kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI/MAJUKUMU.**

- Kuhakikisha mali yoyote ya Ofisi inayotolewa langoni (nje ya ofisi) ina hati na idhini.
- Kuhakikisha kuwa mali yote inayoingizwa langoni inazo hati na uhalali wake.
- Kulinda usalama wa majengo, ofisi na mali za ofisi mchana na usiku.
- Kuhakikisha kwamba wageni wote wanaoingia katika eneo la ofisi wanaidhini ya kufanya hivyo.
- Kupambana na majanga yoyote yatayotokea katika sehemu ya kazi kama vile moto, mafuriko na kutoa taarifa katika vyombo vinavyohusika.
- Kutoa ushauri wa jinsi ya kuboresha huduma ya ulinzi mahali pa kazi.

**MSHAHARA.**

Mshahara kwa nafasi hiyo ni TGOS 'A'

**MASHARTI YA JUMLA.**

- Mwombaji awe raia wa Tanzania na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo, nakala ya cheti cha kidato cha nne naa nakala ya cheti cha kuzaliwa na vithibitishwe na Hakimu/ Wakili anayetambulika na Serikali (True Copies of the orginals).
- Waombaji wote waambatinishe maelezo binafsi yanayo jitoshileza (Detailed Curriculum Vitae) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini wawili (02) na picha moja ‘Passport Size’ za hivi karibuni (ziandikwe jina kwa nyuma)
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 7 Disemba, 2020 saa 09:30 Alasiri.
- Maombi yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo:-


Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

S.L.P 126


**BUNDA.**

Imetolewa na:

  
Stephen S. Ochieng'.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

**BUNDA.**

  
MURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA